

## Haki ya Msingi ya Usawa mbele ya Sheria.

TAWLA ipo kwa kukusaidia wewe kuelewa nini hasa maana ya Haki hii.

Endapo una swali lolote, au unahitaji msaada, tafadhali tuandikie "TAWLA", S.L.P. 9460, Dar es Salaam Tanzania.



DESIGN NA MICHORO WALTER LEMA  
(DESIGN AND DRAWING)  
REDISIGN HELMUT PFINDEL

IMEFADHILIWA KWA PAMOJA  
NA ROYAL DANISH EMBASSY  
IMEFADHILIWA NA MEDICAL MISSION SUPPORT  
UNITED STATES INFORMATION SERVICES (USIS)

# MALEZINA MATUNZO KWA WATOTO



IMETOLEWA NA KUTAYARISHWA NA CHAMA CHA  
WANAWA KE WANASHERIA TANZANIA (TAWLA)

## MALEZI NA MATUNZO YA WATOTO

### Mtoto ni nani

Kisheria Mtoto ni mtu au kijana ambaye ana umri chini ya miaka kumi na minane. Vinginevyo katika hali ya kawaida mtoto ni mtu au kijana ambaye bado kimalezi na kimatunzo yuko chini va himaya ya wazazi au walezi wake.

### Nari ana jukumu la kutoa malezi na matunzo?

Kwa watoto wanaozaliwa ndani ya ndoa, wazazi wote kwa pamoja wana jukumu la kuwalea na kuwapa matunzo watoto hawa kwa kadri ya uwezo wao. Ni kosa la jina i kutokutoa matunzo kwa watoto wako au kuwatelekeza.

### Sheria ya ndoa inasemaje?

Shera hii inatambua jukumu hili muhimu waliloka-bidhiwa wazazi kuwalea watoto wako katika misingi imara. Endapo Wazazi watatengana, Sheria hii inaelekeza kwamba watoto wanaweza kulelewa chini ya malezi ya yeyote kati ya hao wazazi ilimradi tu anayeomba kupewa malezi athibitishwe ana uwezo wa kuwalea watoto husika na kigezo ambacho mahakama zimekuwa zikiturnia ni "maslahi ya mtoto yatawekwa mbele kabisa." Katika msingi huo mara nyingi watoto wachanga watawekwa chini ya uangalizi wa mama yao isipokuwa kama kuna sababu za msingi za kumnyima uangalizi huo.

Hata hivyo matunzo ya watoto yataendelea kuwa majikumumu ya wazazi wote hata baada ya matengano. Pale ambapo watoto watakuwa chini ya uangalizi wa mama, baba atakuwa na jukumu la kupeleka pesa za matunzo kutegemeana na kipato alicho nacho au mahakama itakavyokuwa imeamuru.

### Je watoto waliozaliwa nje ya ndoa wana haki zozote?

Sheria inamtambua mtoto aliyezaliwa nje ya ndoa kuwa ni mtoto wa upande wa kikenki (mtoto wa mama). Hata hivyo endapo baba wa mtoto huyu atajitambulisha na hivyo kulea mimba na baadaye kumtunza mtoto anayezaliwa, basi mtoto huyu atambuliwa kuwa ni wa baba huyu hata kama hawa wazazi wawili hawataungana pamoja katika ndoa. Baba huyu atategemewa kama vile baba wa ndoa kuendelea kumtunza mtoto wake huyo aliyezaliwa hadi aweze kujitegemea mwenyewe.

Katika hali nyingine, baba anaweza kumhalalisha mtoto wake aliyezaliwa nje ya ndoa ilimradi tu aliipe faini inayopaswa chini ya sheria za kimila zinazosimamia maswala ya namna hii.

Pale ambapo baba anakana kuhusika na mtoto aliyezaliwa mama muhusika anayo haki ya kupeleka mashitaka mahakamani kumtaka baba muhusika awajibishwe kwa vitendo-vyake ili aweze kumtunza mtoto aliyezaliwa. Tatizo kubwa hadi sasa ni kwamba matunzo yaliyoidhinishwa na Sheria ni kiwango kidogo cha shs. 100 tu. Hata hivyo mahakama zinaangalia uwezo wa mtu.

### Izingatiwe

Ni kosa la jinai kutotoa matunzo au kuwatelekeza watoto iwe ni wale waliozaliwa ndani au nje ya ndoa.

